

Swahili

iHealth®
COVID-19
Antigen Rapid Test

**Self-Test
At Home
Results In
15 Mins**

Maelekezo ya Matumizi ya Kipimo cha Haraka cha Antijeni ya UVIKO-19

Hatua ya 1: Andaa Nyenzo


Step 1: Prepare Material

Unaweza kuwa na Seti ya 1 ya Kipimo au Seti ya 2 ya Kipimo ndani ya pakiti. Tafadhalli fuata hatua sahihi kulingana na seti husika uliyopokea.

SETI YA 1 YA KIPIMO:

Test Set 1:

Fungua pakiti, chukua Kadi ya Kipimo ya UVIKO-19 ndani ya pochi, Tyubu iliyojazwa kabla mchanganyiko wa kufyonzea na Kifutio. Pindi upo tayari kuendelea na kipimo, fungua pochi ya folii ya Kadi ya Kipimo ya Uviko-19.



1 COVID-19 Test Card
in Pouch



1 Empty Tube and
1 Sealed Solution



1 Swab

SETI YA 2 YA KIPIMO:

Test Set 2:

Fungua pakiti, chukua Kadi ya Kipimo ya UVIKO-19 ndani ya Pochi, Tyubu tupu, Mchanganyiko uliyofungwa, na Pamba. Pindi upo tayari kuendelea na kipimo, fungua pochi ya folii ya Kadi ya Kipimo ya Uviko-19.



1 COVID-19 Test Card
in Pouch



1 Pre Filled Tube



1 Swab

Hatua ya 2: Kusanya Sampuli

Step 2: Collect Sample

A. Ondoa pamba kutoka kwenye pakiti yake, kuwa mwangalifu kutokugusa ncha ya pamba. Tafadhalli itunze pakiti ya pamba kwa matumizi ya baadae.

B. Taratibu ingiza ncha yote ya pamba inayofyonza (mara nyingi $\frac{1}{2}$ hadi $\frac{3}{4}$ ya inchi) ndani ya pua yako.

C. Taratibu na polepole sugua ndani ya pua katika mjongo wa mduara dhidi ya ukuta wa pua kwa walau mara 5. Chukua walau sekunde 15 kukusanya spesimeni na kuwa na uhakika kukusanya majimaji yoyote ya pua kwenye pamba. Kwa kutumia pamba hiyo hiyo, rudia utaratibu huo huo wa ukusanyaji sampuli kwa pua nyingine. Kuwa na uhakika kusugua pua ZOTE kwa PAMBA HIYO HIYO.



Hatua ya 3: Chakata Sampuli

Step 3: Process Sample

A. Iweke tyubu kwa uwima kwenye meza na pindisha kifuniko kikubwa cha rangi ya machungwa kufungua tyubu.

B. Ingiza pamba ndani ya tyubu, gusa chini ya tyubu kwa ncha ya pamba, na changanya kwa walau mara 15.



A



B




Stir x15

C

C. Minya pande za tyubu kutoa kimiminika kingi kadri iwezekanavyo kutoka kwenye pamba na halafu itoe pamba.

D. Urudishie mfuniko mkubwa wa rangi ya machungwa, rudisha pamba katika pakiti. Utupaji salama wa pamba na pakiti.



C



D



Hatua ya 4: Ongeza Sampuli

Step 4: Add Sample

Pindisha kufungua kifuniko kidogo cheupe cha tyubu. Ongeza matone 3 ya sampuli kwenye Sehemu ya Sampuli ya Kadi ya Kipimo ya UVIKO-19. Urudishe mfuniko mdogo mweupe.



Hatua ya 5: Subiri dakika 15

Step 5: Wait 15 minutes

Anzisha muda kwa kubofya kitufe cha "Start Timer" kwenye Aplikesheni, mara tu baada ya kuongeza sampuli kwenye Sehemu ya Sampuli. Matokeo yatakuwa tayari ndani ya dakika 15.




Hatua ya 6: Soma Matokeo

Step 6: Read Results

Matokeo hayapaswi kusomwa baada ya dakika 30 (Matokeo yallyoonyeshwa kwenye ukuzwaji 2X).



Look carefully for a C line here.



Look carefully for a T line here.

Hatua ya 7: Maelezo ya matokeo ya Kipimo

Step 7: Test Result Explanation

Matokeo Chanya:

Matokeo CHANYA lazima yaonyeshe KWA PAMOJA mstari wa C (ZAMBARAU MPAUKO) na mstari wa T (ZAMBARAU ILIYOKOLEA). Matokeo chanya humaanisha kuwa antijeni za virusi kutoka kwenye UVIKO-19 zilligundulika na mtu huyo ana UVIKO-19. Watu wenyewe matokeo chanya wanapaswa kujitenga na kutafuta huduma ya ufuatilaji kwa daktari au mtaalamu wao wa huduma za afya kwa maana upimwaji wa nyongeza na kuripoti afya ya Jamil kunaweza kuwa ni lazima.

Positive Result



Matokeo Hasi:

Matokeo hasi yataonyesha TU mstari wa C (ZAMBARAU MPAUKO).

Negative Result



Matokeo hasi humaanisha kuwa antijeni za virusi kutoka kwenye UVIKO-19 hazikugundulika na kwamba mtu huyo anafikirika kuwa hana UVIKO-19.

- Tafadhalli kumbuka kuwa matokeo hasi hayaondoi UVIKO-19
- Ikitokea matokeo hasi ya kipimo: Endelea kufuata mapendekezo yote ya kuweka umbali kati ya watu, na chukua njia za kujilinda. Kama makisio ya maambukizi yanaendelea na/au kipimo chako cha kwanza ni hasi, rudia kipimo baada ya siku 1-2 na muone mtaalamu wako wa huduma za afya au kituo cha UVIKO-19 cha karibu yako.

Hatua ya 8: Tupa Kifaa cha Kipimo

Step 8: Dispose of Test Kit

Baada ya kipimo kukamilika, tupa vifaa vya kipimo katika sehemu ya takataka

See more at
AnchoragePLNs.org



This project was partially supported by a grant awarded by the Municipality of Anchorage, Anchorage Health Department. The opinions, findings, conclusions or recommendations expressed in this publication are those of the author and do not necessarily reflect the views of the Municipality of Anchorage, Anchorage Health Department.